# Majukumu na Athari za Nyimbo za Watoto katika enzi za Teknolojia ya Kidijiti: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto nchini Tanzania

*Steven Elisamia Mrikaria*

**Ikisiri**

Karne ya 21 ina maendeleo makubwa katika nyanja ya sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano. Ni katika karne hii ambapo fasihi simulizi ya Kiswahili imeshuhudia kuingia kwa mambo mengi mapya yaliyougusa utanzu wake mkubwa na wa awali kabisa wa nyimbo za watoto za Kiswahili kiasi cha kuathiri uhalisia wake. Makala haya yanaangalia namna maendeleo ya teknolojia ya kidijiti yanavyoathiri nyimbo za watoto. Makala pia yanagusia kwa kifupi mustakabali wa nyimbo za watoto.

## 1.0 Utangulizi

Kati ya vipindi ambavyo havitasahaulika katika historia ya fasihi simulizi ya Kiswahili ni karne ya 21. Karne hii imeshuhudia kuingia kwa mifumo mingi mipya, yenye kujikita katika urahisishaji wa kiutendaji wa fasihi simulizi. Mambo haya mapya yamejitanzua kupitia maendeleo ya teknolojia yaliyopelekea kuibua kwa mfumo wa teknolojia ya kidijiti. Mfumo huu, uliotokana na matumizi ya teknolojia na vyombo vya kielektroniki, umeingia, ukatandawaa na hata kukita mizizi yake katika fasihi simulizi ya Kiswahili, nyimbo za watoto za Kiswahili zikiwemo. Ifahamike kwamba, nyimbo hizi za watoto zilizokuwa zikijenga uhusiano mwema miongoni mwa watoto na jamii, zimejikuta zikiangukia katika dimbwi la maendeleo ya kidijiti, na hivyo kuzua wasiwasi miongoni mwa wataalamu wa fasihi simulizi. Ndipo tunaposukumwa kutathmini jinsi nyimbo za watoto za Kiswahili zilivyoingiliwa na mfumo huu na kujadili athari zake kiutamaduni, kiutungaji, kiutendaji na kadhalika. Kabla ya kujadili athari hizo, makala yatapitia kazi mbalimbali za nyimbo za watoto na kufafanu dhima zake kwa jamii.

## 2.0 Nyimbo za Watoto za Kiswahili nchini Tanzania

Ingawa ni vigumu kupata chanzo halisi cha nyimbo za watoto (taz. Mulokozi, 1975; Iona na wenzake, 1997; Cuddon, 1998), nyimbo hizi zimekuwepo katika jamii kwa muda mrefu sana kama sehemu ya fasihi simulizi ya jadi. Kwa kuwa fasihi simulizi ni utanzu hai (Rubanza, 1994; Mulokozi, 1996; Samwel 2012), nyimbo za watoto-kama utanzu wa fasihi simulizi-zimekuwa zikizaliwa, kukua na hata kufa. Mara nyingine, pamoja na nyimbo hizi kuwa za watoto, baadhi yake zimekuwa zikiimbwa na hata watu wazima kutokana na umuhimu wake kwa wanajamii. Kutokana na umuhimu huo wataalamu mbalimbali wamejitokeza kuzitafiti na kuziandikia nyimbo hizo kwa malengo mbalimbali. Miongoni mwao ni pamoja na Mulokozi (1975, 1987 na 1996), Ndumbaro (1981), Balisidya (1987), Matteru (1989), Msokile (1992), Senkoro (1996), Wamitila (2003), Ngure (2003), King'ei (2005) na Omari (2008).

Mulokozi (1975) katika andiko lake anasema kuwa ingawa nyimbo hizo zinaimbwa na watoto wakijifurahisha, zinabeba ujumbe muhimu katika kuyaongoza mawazo yao katika masuala muhimu yahusuyo jamii yao. Anafafanua kuwa, ni vigumu sana kuelewa asili ya kila wimbo kwani kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi simulizi, nyimbo za watoto huibuka na hubadilika kutokana na wakati na mazingira. Kwa upande wake Ndulute (1977) anazichukulia nyimbo za watoto kuwa ni zile zinazoimbwa na watoto wakiwa shuleni au katika michezo yao ya kila siku. Anasema kuwa watoto wanapokuwa katika michezo yao huimba nyimbo ambazo huzikumbuka hata wanapokuwa watu wazima.

Halikadhalika, Balisidya (1987) ameziangalia nyimbo za watoto za Kiswahili kwa kukiri kuwepo kwa nyimbo hizo katika jamii. Katika kazi yake Balisidya anasema kuwa nyimbo za watoto zimekuwepo katika jamii tangu zamani, na zimekuwa zikiimbwa zikipokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mawazo haya hayana tofauti na ya Mulokozi (1975) ila yanatusaidia kubaini kwamba nyimbo za watoto zinarithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Vilevile, yanashadidia kwamba, jamii ikibadilika basi na hata nyimbo za watoto katika jamii hiyo hubadilika. Hoja hii itatusaidia katika kujadili mabadiliko ya kiutendaji ya nyimbo za watoto za Kiswahili katika kipindi hiki cha maendeleo ya kidijiti.

Mbarouk (1981) katika utafiti wake wa nyimbo za michezo ya watoto amegundua kuwa nyimbo za watoto ni burudani kwa watoto na hutumia lugha rahisi yenye kueleweka na aghalabu isiyokuwa na tamathali za semi. Mbarouk anasisitiza kwamba nyimbo hizi ziimbwe kwa kuzingatia matumizi ya lugha ya Kiswahili. Bila shaka Mbarouk alishatishwa na matumizi makubwa ya lugha ya Kiingereza katika nyimbo za Kiswahili na kasumba kwamba kujua Kiingereza ndiko kustaarabika. Mbarouk anaibuka na mawazo kwamba mafunzo na ujumbe uliomo katika nyimbo hizo huwafikia watoto kwa haraka zaidi kwa kutumia lugha yao waliyoimilisi. Mawazo ya Mbarouk (1981) yanakaziwa na Rwilomba (1994) aliyetafiti matumizi ya sanaa za maonesho kama njia ya kufundishia masomo ya Hisabati na Kiingereza katika shule za awali na msingi. Rwilomba aligundua kwamba nyimbo za watoto za Kiswahili zina mchango mkubwa katika kutolea maarifa ya masomo mengine kwa watoto. Hivyo, nyimbo za watoto husaidia kufundishia na kujifunzia kwa watoto.

Kayoka (1994) anayaunga mkono mawazo ya Mbarouk (1981) na Rwilomba (1994) kuhusiana na uwezo wa nyimbo za watoto katika kurahisisha ujifunzaji na ufundishaji wa masomo kwa watoto. Anatolea mfano wa jinsi nyimbo hizo zinavyoweza kutumika katika kufundishia dhana za kibiolojia katika shule za msingi. Kayoka anaongezea faida nyingine kuwa, hupunguza utawala wa mwalimu darasani na kutoa uhuru kwa wanafunzi kujifunza zaidi kwa kutumia vionjo vya milango ya fahamu.

Msokile (1992) anaendelea kufafanua kwamba kwa kawaida nyimbo za watoto za Kiswahili huongelea mazingira wanayoishi na kucheza watoto na kwamba zina dhima kubwa. Hapa Msokile anasisitiza kuwa kusambazwa kwa nyimbo hizo kutoka kizazi kimoja hadi kingine kunasababisha mabadiliko ya nyimbo sambamba na mabadiliko ya kijamii. Hata hivyo, Msokile anatahadharisha kwamba wakati mwingine nyimbo hizi hazina maana kabisa lakini huimbwa tu ili kuiburudisha hadhira yake. Pia, anasisitiza kwamba, miongoni mwa mambo mengine, nyimbo hizi ni muhimu sana katika jamii kwani zinaelimisha, zinaburudisha, zinahuzunisha na zinaweka wazi mambo mbalimbali katika jamii.

Senkoro (1996) anaangalia nyimbo za kubembeleza watoto, yaani bembezi, na anaeleza jinsi nyimbo hizo zinavyoakisi masuala ya kijinsia na uhalisi wa maisha katika jamii. Anasema kuwa nyimbo hizi hutumiwa kuelezea mitazamo ya wabembelezaji kuhusu ulimwengu, ndoa na waume. Pia, huelezea hofu, malalamiko, uchungu, hasira na matumaini yao. Anasisitiza kuwa katika jamii za mfumo jike kama zile za Wakaguru nyimbo hizi zinaonesha umuhimu wa kijamii wa mwanamke kama kiumbe huru anayeshiriki sawa na kikamilifu katika shughuli za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Senkoro anaendelea kusema kuwa bembezi kutoka pwani ya Afrika ya Mashariki, ambapo mfumo wa kikabaila na dume umejikita, zinaonesha picha ya utumwa, umaskini na ukosaji wa haki za kijamii.

Omari (2008) amechunguza nyimbo za watoto kwa kutilia mkazo namna watoto wanavyochorwa na kushirikishwa kimajukumu katika muktadha wa kumjenga mtoto kiakili na kimatendo. Katika uchambuzi wake huo anatuangazia kwamba kuna haja ya kuzisikiliza nyimbo hizi kwa kuwa, mbali na kutoa burudani, hubeba ujumbe unaohitaji kuchambuliwa kitaalamu. Mawazo yake yanatusukuma kuzichambua baadhi ya nyimbo za watoto za Kiswahili na kubainisha jinsi zinavyopitisha ujumbe muruwa kwa jamii zinazozisikia nyimbo hizo. Tutayaendeleza mawazo ya Omari kwa kujikita katika kuchanganua utendaji na mustakabali wa nyimbo hizo katika mfumo wa teknolojia ya kidijiti. Hii inatokana na ukweli kwamba mfumo huu ndio unaoongoza katika kuyateka, kuyajenga na hata kuyabomoa mawazo na matendo ya watoto ulimwenguni kote.

Mawazo ya wataalamu na watafiti tuliowajadili yanatudhihirishia kwamba nyimbo za watoto, ambazo wengi wetu tumeziimba utotoni tukiwa michezoni au shuleni, zina ufundi mkubwa wa kisanaa na maudhui anuwai. Tumebaini kwamba nyimbo za watoto, kama tanzu nyingine za fasihi simulizi, zinaenda sanjari na jamii zinamoimbwa na hivyo hubadilika kulingana na mabadiliko yanayotokea katika jamii. Tunamaanisha kwamba wakati wa ukoloni nyimbo za watoto ziliakisi hali hiyo. Bila shaka utendaji, fani na maudhui yake ulibadilika kusawiri hali halisi ya mfumo wa ukoloni, ila kutokana na utafiti wetu hakuna mahali panapotuthibitishia hili. Wakati

wa uhuru hali ya nyimbo za watoto ilikuwa ikiendelezwa jinsi hiyohiyo na hata wakati wa utandawazi.

## 3.0 Majukumu ya Nyimbo za Watoto katika Jamii

Kiputiputi (2011) anatufafanulia dhana ya dijiti kuwa ni kugeuza chanzo data za analogia kama vile sauti na kuwa katika umbo la dijiti ili iweze kuchakatwa na kompyuta. Kwa maelezo haya ya Kiputiputi tunafasili kuwa teknolojia ya kidijiti kuwa ni ule uwezo wa kuzigeuza data fulani, ikiwa ni pamoja na data za kifasihi (kuanzia sasa nyimbo za watoto za Kiswahili), kuwa katika umbo bora zaidi linaloweza kuangaliwa na jumuiya au vikundi vya kijamii kwa uwazi zaidi. Katika kuzibadilisha nyimbo za watoto za Kiswahili ili zikidhi matakwa ya teknolojia ya kidijiti, ni lazima nyimbo hizo ziwekwe katika mitandao au vifaa vya kisasa vya kuhifadhia ambavyo ni redio, televisheni, kompyuta, kanda za video, sidi, dividi, visidi, *iPad, Kindle*, *You Tube*, *Facebook*, *Twitter*, na vifaa vingine vya kidijiti.

Mchakato wa kuiendesha dunia kwa kupitia teknolojia ya kidijiti umeleta na kueneza mwingiliano unaofanana na huo katika fasihi simulizi ya Kiswahili, ambapo karibu mataifa yote yamekuwa yakibadilishana kazi za fasihi kwani teknolojia hii haifungwi na mipaka ya kinchi. Kwa kutumia teknolojia hii, inayoifanya dunia kuwa kama kijiji kimoja, dunia imejikuta ikishirikiana kazi za fasihi ikiwa ni pamoja na nyimbo za watoto. Mawazo haya yanathibitishwa na Mutembei (2006) na Mrikaria (2007). Nyimbo za watoto, zilizomo katika teknolojia ya kidijiti hutarajiwa kusambaza majukumu mbalimbali kwa watoto na jamii. Miongoni mwa majukumu hayo ni kama ifuatavyo:

### 3.1 Kuwajenga Watoto Kiakili na Kifikra

Nyimbo za watoto za Kiswahili ni sanaa yenye uwezo wa kuwajenga watoto kiakili na kuwafanya waweze kufikiri na kukumbuka mambo mbalimbali kwa urahisi. Nyimbo hizi huwasaidia watoto kudadisi jambo, kulikumbuka na kulitekeleza. Halikadhalika, huwafanya kushika kwa urahisi majaribio mbalimbali kutokana na uwezo wake wa kujifunza kuwa mpana. Hapa tuna maana kwamba, mtoto anajifunza vitu vingi kwani hutumia uwezo na nguvu kidogo katika kujifunza tofauti na atakapofundishwa kwa njia ya kuandika tu. Mfano mzuri wa jinsi nyimbo hizo zinavyoweza kuwajenga watoto kiakili na kifikra unaonekana katika wimbo uitwao *Mabata madogo*:

1. Mabata madogodogo yanaogelea
yanaogelea katika shamba zuri la bustani
Yanapenda kutembea bila ya viatu
Yanapenda kulia kwakwa kwa kwaaaa
Kwa kwa kwa kwaaa...

Wimbo huu tunaona kwamba unamfundisha mtoto tabia za ndege aina ya bata, kulia kwake, kutembea kwake na hata kutenda kwake. Wimbo kama huu unapotumika mara kwa mara humkumbusha mtoto tabia za bata hata bila kumwona.Wimbo mwingine unaofanana na huu, ambao nao una dhima ya kumwelimisha mtoto tabia za viumbe mbalimbali ni *Kipepeo:*

2. Kipepeo anaruka
Anaruka anaruka,
Anatafuta chakula...

Hapa tunaona kwamba watoto wanafunzwa matendo na tabia za vipepeo, kwamba hurukaruka huku na huko kutafuta chakula. Kupitia wimbo huu mtoto pia huweza kujifunza kwamba katika mapambano dhidi ya maisha, viumbe (wanyama, wanadamu na wadudu) hawana budi kuhangaika kujitafutia riziki (chakula). Wimbo huu unamwandaa mtoto kupambana na mazingira yake na kuwa tayari kuhangaika katika kutatua matatizo mbalimbali yanayomkabili.

### 3.2 Kuwafunza na Kuwaendeleza Watoto Kimaadili

Nyimbo za watoto zinafundisha maadili mema na tabia zinazokubalika katika jamii. Miongoni mwa mambo ya kimaadili ambayo mtoto huweza kujifunza kupitia nyimbo ni heshima kwa wakubwa, kusema asante apewapo kitu chochote, kutoharibu vitu na maadili juu ya kuthamini vitu na viumbe ambavyo ni hazina kwa jamii. Kupitia wimbo tuliounukuu katika data namba (2) tunaona kwamba mtoto anajifunza kuwa kipepeo harukiruki bila sababu bali anaruka akitafuta chakula. Hapa mtoto anaadilishwa kutomuua kipepeo kwani anakuwa katika harakati za kuhangaika apate chakula ili asife kwa njaa. Aidha, kupitia wimbo huo mtoto anaweza kujifunza kwamba shughuli ya kutafuta chakula huambatana na kazi ngumu, hivyo kujengewa moyo wa kuwaheshimu wazazi na walezi wake ambao wanamtafutia chakula.

Uwezo wa nyimbo za watoto kuadilisha unaonekana pia katika wimbo wa *Mabata Madogo* tuliounukuu katika data namba (1). Katika wimbo huo, mtoto anaangalizwa juu ya tabia ya uchafu ya bata ya kuogelea, hata kwenye maji machafu, na kutembea bila viatu! Kupitia wimbo huu mtoto anafundishwa kutopenda kucheza au kutembea bila kuvaa viatu. Ifahamike kwamba watoto wengi hupenda sana kuchezea maji machafu na hivyo kuwa kwenye hatari ya kupata magonjwa kama vile kuharisha na kuhara damu, homa ya matumbo, minyoo na kadhalika. Ni kwa kupitia wimbo huo, mtoto anaadilishwa kutotembea bila kuvaa viatu. Bata anachorwa kama kiumbe mchafu anayetembea bila viatu. Hivyo, matumizi ya mabata wadogo katika wimbo huu si ya kibahati nasibu bali ni ya kimakusudi. Mabata madogo ni sitiari ya watoto wadogo. Mabata wakubwa pia huogelea bila viatu lakini hapa msisitizo ni mabata wadogo, yaani watoto wadogo. Kutovaa viatu ni tabia mbaya ambayo mtoto hapaswi kuwa nayo kwani inamweka katika hatari ya kuchomwa na miba, misumari na hata kupata maambukizi kama vile fangasi na kadhalika.

Wimbo mwingine ambao unamwadilisha mtoto unaitwa *Yai Bovu*. Kupitia wimbo huo mtoto anafundishwa kwamba yai bovu linanuka na hivyo halipaswi kutunzwa bali kutupwa jalalani. Yai bovu hapa ni kielelezo cha vitu vyote visivyofaa kwa matumizi. Hivyo kupitia wimbo huu mtoto anaadilishwa juu ya umuhimu wa tabia ya usafi. Rejelea wimbo huo:

3. Yai bovu yai bovu,
linanuka linanuka. linanukaje linanukaje
ho ho ho, watoto msitazame nyuma
yai bovu linapita...

### 3.3 Kuwaburudisha, Kuwastarehesha na Kuwafundisha Watoto

Mulokozi (1996) anatutanabahisha kuwa nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa katika jamii za Kiafrika. Anafafanua kwamba zinaweza kutumika kuwaburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko. Kwa kuzingatia maelezo hayo ya Mulokozi, watoto wanapokuwa shuleni, huimba kwa mazoea bila ya kufahamu kuwa wanajiburudisha na kujifunza mambo mbalimbali. Wakati mwingine, nyimbo hizi humshirikisha mtoto na viungo vyake vya mwili wakati wa kuimba na kutenda. Kwa mfano, katika wimbo wa *Mabata Madogo* (1) tunaona kwamba wakati wa uimbaji wake watoto hufundishwa kuigiza matendo ya mabata wadogowadogo wanaotembea bila viatu. Hapa mtoto huigiza kama bata atembeavyo bila viatu kwa kupiga miguu yake chini na kulia kwakwa kwaaa kwa na kupiga mikono yao ubavuni mwa tumbo. Kwa kufanya hivyo mtoto huchangamshwa na kuburudishwa. Tunapouangalia wimbo wa *Nyuki Lia* tunaona ukidhihirisha jukumu la nyimbo la kumburudisha na kumstarehesha mtoto. Maneno ya wimbo huo yanasema:

4. Zum zum zum we mama nyuki lia wee,
Ruka mbali kutafuta ua zuri kwa chakula
Zum zum zum we mama nyuki lia weee....

Wimbo huu huimbwa na kuchezwa kwa namna mbili. Moja ni kwa kushikana mikono kwa kufinyana. Namna ya pili ni kwa kutengeneza duara kubwa, katikati huwekwa viti ambavyo hukaliwa waanzapo kuzunguka na wamalizapo wimbo. Watoto husimama na kuimba kisha kukalia viti hivyo wamalizapo wimbo. Huendelea hivyo hivyo kwa kupunguza kiti kimoja kimoja mpaka mwisho na atakayeweza kukalia kiti cha mwisho ndiye mshindi wa mchezo na hupongezwa. Hivyo, mchezo huu pamoja na kutoa burudani humpa mtoto moyo wa ushindani ambao humpa motisha katika masomo yake. Wimbo *Nampenda Shuadina* pia humburudisha mtoto. Maneno yake ni:

5. Nampenda shuadina shuadina shuadina,
mama yake simjui simjui simjui
anatoka sehemu gani sehemu gani...

Wimbo huu, kama zilizotangulia, huimbwa kwa kuigiza matendo ya mwili. Vitendo hivyo ni pamoja na kuchezesha kiuno ambacho hushikwa kwa mkono mmoja na

mwingine hushika kichwani. Kwa kucheza hivyo mtoto huchangamshwa na kuondolewa uchovu aliokuwa nao awali. Hivyo nyimbo nyingi za watoto hujengwa katika muktadha na madhumuni ya kumstarehesha na kumburudisha mtoto.

### 3.4 Kuwajengea Watoto Moyo wa Uzalendo

Jukumu jingine la nyimbo za watoto ni kuwajengea watoto moyo wa uzalendo. Pindi mtoto aimbapo nyimbo za kuhamasisha jambo fulani ni dhahiri kuwa atakuwa anajifunza kwa dhamira ya uzalendo wa kupenda kitu au nchi yake. Kwa mfano, wimbo *Tanzania Tanzania* unahamasisha uzalendo wa kuipenda Tanzania na watu wake wakati wote. Ingawa wimbo huu si wa watoto hata hivyo hutumiwa sana shuleni kuendeleza dhana hiyohiyo ya uzalendo wa kitaifa.

6. Tanzania Tanzania, nakupenda kwa moyo wote
Nchi yangu Tanzania, jina lako ni tamu sana
Nilalapo nakuota wewe...

Sote tunafahamu kwamba Tanzania ina jamii nyingi na kila jamii (kabila) ina nyimbo zake ambazo hutumika katika kuhamasisha watu wake masuala mbalimbali. Ila nyimbo hizo kwa mfano *Tanzania Tanzania* na hata Wimbo wa Taifa zinawasukuma watoto kusahau tofauti zao na kuwa makini katika kulitangaza na kulitetea taifa au nchi yao kila wanapotakiwa kufanya hivyo.

### 3.5 Kuwafunza Matamshi na Kuwajengea Watoto uwezo wa Uvumbuzi

Nyimbo huweza kumfunza mtoto kutamka maneno na kumjengea uwezo wa kuvumbua mambo mapya. Katika hili, nyimbo zifundishwazo shuleni zimelenga kumpatia mtoto kujua vitu mbalimbali katika mazingira yake. Kwanza tunaona mtoto anapoziimba hujifunza kutamka na kumfanya awe mwepesi katika kuzungumza, kuongeza misamiati ndani ya ubongo wake na ndipo aanze kuunganisha hiyo misamiati na kuandika. Humwezesha pia kujua majina ya vitu mbalimbali kama meza, magari, nyumba, viti, nyoka n.k. Mfano wa nyimbo hizi ni pamoja na *Kipepeo*, *Ndizi Machungwa*, *Mabata Madogo*, *Chei Chei Shangazi*, *Yai Bovu* na *Simama Kaa rukaruka*.

Wataalamu wa elimu wanathibitisha kwamba hatua ya kwanza katika kujifunza na kufundisha ni kutamka na kisha kuandika hufuata. Hivyo kwa mtoto kuanza kuimba nyimbo hizi anajifunza sauti mbalimbali za lugha husika na hatimaye hujifunza kuziandika. Kwa msingi huo, tuliyoyataja hapo juu ni baadhi tu ya dhima za nyimbo za watoto kwa watoto wenyewe na kwa jamii pia. Sehemu inayofuata inajadili mchango wa teknolojia ya kidijiti katika nyimbo za watoto za Kiswahili.

## 4.0 Athari za Teknolojia ya Kidijiti katika Nyimbo za Watoto za Kiswahili

Teknolojia ya kidijiti ina athari mbalimbali katika nyimbo za watoto za Kiswahili. Ufafanuzi wa athari hizo ni kama ifuatavyo:

### 4.1 Huathiri Uhai wa Utendaji wa Nyimbo

Athari ya kwanza muhimu inayoonekana kutokana na matumizi ya teknolojia ya kidijiti katika nyimbo za watoto za Kiswahili ni kuifanya fasihi hiyo kuwa si hai. Uhai wa fasihi simulizi hutokana na, pamoja na mambo mengine, kukutana kwa fanani na hadhira ana kwa ana na uwezo wa hadhira kuchangia na kushiriki katika utendaji wa utanzu husika. Aidha, uhai wa fasihi simulizi hutokana na uwezo wa fanani kubadilisha utendaji wake kulingana na hali ya hadhira. Kama hadhira imechoka fanani atapaswa kubadilisha utendaji wake ili kuifanya hadhira yake ichangamke tena. Sifa hizi zote zimeondolewa na matumizi ya teknolojia ya kidijiti katika nyimbo za watoto za Kiswahili. Pindi nyimbo za watoto zinapohifadhiwa katika vifaa vya kiteknolojia basi hadhira na fanani hutenganishwa.

Utendaji wa nyimbo za watoto za Kiswahili katika teknolojia ya kidijiti kunamfanya fanani kuwa si 'halisi'. Fanani hawezi kubadilisha utendaji wake kulingana na hali ya hadhira. Tunamaanisha kwamba, kazi ikisharekodiwa katika kanda za kaseti, sidi, dividi au njia nyinginezo hutendwa kwa namna moja kwa hadhira za aina zote bila kujali hali, umri, uwezo wa kiakili na kadhalika. Hivyo ufaraguzi wa fanani hupungua na kuathiri fani na maudhui ya nyimbo husika. Aidha, matumizi ya baadhi ya vifaa kama vile kanda za kaseti hufanya matendo yanayoambatana na utendaji wa nyimbo husika kutoonekana na hivyo kukwamisha upatikanaji wa maudhui yake. Finnegan (1970), Mulokozi (1996) na Samwel (2012) wanasisitiza kwamba matendo ni muhimu sana katika uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi *ikiwa ni pamoja na nyimbo za watoto* (msisitizo ni wetu).

### 4.2 Huathiri Umiliki wa Nyimbo

Mbali na athari katika uhai wa nyimbo za watoto za Kiswahili, teknolojia ya kidijiti imeathiri sana umiliki wa nyimbo za watoto za Kiswahili. Sifa muhimu ya nyimbo za watoto ni za kimapokeo. Mulokozi (1996) na King'ei (2005) wanaeleza kwamba, nyimbo za mapokeo ni nyimbo za jamii ambazo hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa kuzingatia mgawanyo wa nyimbo uliofanywa na Mulokozi (1996) nyimbo za watoto za mwanzo zilikuwa ni zao la jamii na hivyo haikuwa rahisi kumjua mtunzi halisi wa nyimbo hizo. Zilikuwa ni mali ya jamii nzima kwani kila mmoja alikuwa akizisikiliza na kwenda kuziimba mahali pengine bila kuhitaji ruhusa ama kibali kutoka kwa mtu yeyote ndani au nje ya jamii yake. Angalia wimbo wa

*Ukuti Ukuti:*

7. Ukuti ukuti (Kiitikio) wa meme wa meme

Mwenzetu mwenzetu " kagongwa kagongwa
Na nini na nini? " na gari na gari
Tumpeleke hospitalini sije kusema kwa baba yake
Yesa yesa yesa, Yesa yesa yesa YEEEEEE

Wimbo huu huimbwa na watoto takribani wa jamii zote zinazoongea lugha ya Kiswahili. Ulianza kuimbwa sehemu zenye kulima zao la minazi na kusambaa katika jamii nyingine kwa malengo yaleyale ya kimapokeo. Katika wakati huu wa maendeleo ya teknolojia ya kidijiti, maneno ya nyimbo za watoto za Kiswahili yameonekana kuingizwa katika ghani (*rap*) za wanamuziki wengi wa muziki wa kizazi kipya na muziki wa dansi. Kwa mfano, msanii Ramadhani Masanja (anajulikana pia kama Banza Stone) katika nyimbo nyingi alizoimba akiwa katika bendi ya Tanzania One Theatre (TOT) kama vile wimbo wa *Mwanakwetu* anatumia nyimbo za watoto katika ghani zake. Katika nyimbo zake nyingi, hupenda kutumia maneno ya nyimbo za watoto na hasa nyimbo *Yai Bovu* na *Ukuti Ukuti* tulizozinukuu hapo awali katika data namba (3) na (7). Msanii mwingine aliyezitumia nyimbo za watoto katika ghani na nyimbo zake ni Lucas Mkenda (anajulikana pia kama Mr. Nice). Mwanamuziki huyu kwa hakika ndiye aliyeweka matumizi makubwa sana ya nyimbo za watoto katika nyimbo zake. Yeye ndiye aliyeziimba nyimbo kama vile *Mama*, *Ana Do* na *Kidali Po*, ambazo asili na hata majina yake ni nyimbo za watoto (Omari, 2009). Katika muktadha huo, nyimbo za watoto zimeonekana kubadili mwelekeo wake na kumilikiwa na watu wachache. Nyimbo hizo sasa zimerekodiwa na kuhifadhiwa katika vifaa ambavyo wanajamii wanapaswa kuvinunua ili kuzisikiliza. Hivyo, ili mtu mwingine aweze kumiliki nyimbo hizo, hulazimika kumiliki vifaa vya kidijiti.

### 4.3 Husaidia Uhifadhi wa Nyimbo za Watoto

Uhifadhi wa nyimbo za watoto za Kiswahili za mwanzo ulihusisha zaidi akili ya mtoto kwa kuwa nyimbo hizi zilihifadhiwa kichwani na ziliirithishwa kwa njia ya mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kama Muhando na Balisidya (1976) wanavyosema kuwa nyimbo za watoto ni aina maalumu ya masimulizi zipatikanazo katika fasihi asilia ya jamii yetu, fasihi ambayo inatumia zaidi akili na ubongo wa mwanadamu kwa kuhifadhiwa kwake. Utaratibu huu wa uhifadhi wa nyimbo za watoto ni tofauti na uhifadhi wa nyimbo za watoto katika mfumo wa teknolojia ya kidijiti. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, maendeleo ya sayansi na teknolojia yamesababisha kuwepo kwa vifaa tofauti tofauti vilivyosababisha nyimbo hizi kuhifadhiwa kwenye vifaa kama vile vinasa sauti, kanda za video na vifaa vingine vingi vya kidijiti. Uhifadhi huu, kama tulivyodokeza hapo awali, una athari katika uhai wa nyimbo hizo za watoto. Hata hivyo hii husaidia kufanya kazi hizo kudumu kwa muda mrefu ambapo watoto hawa huweza kuzijifunza kila wanapohitaji kufanya hivyo.

## 4.4 Huathiri Uwasilishaji wa Nyimbo za Watoto

Uwasilishwaji wa nyimbo za watoto za Kiswahili ulikuwa ukifanywa kwa njia ya uimbaji wa mdomo wa ana kwa ana kati ya fanani na hadhira. Hadhira ilikuwa ikimuunga mkono fanani moja kwa moja kwa kupiga makofi, vigelegele, mbinja, kucheka na kadhalika. Aidha, katika uimbaji, fanani husimamia nafasi za wahusika wote katika nyimbo ambapo mtambaji huongoza kwa kutumia ubadilishaji wa sauti, matumizi ya mikono, macho na viungo vingine vya mwili ili kutoa mvuto wa wimbo wake (King'ei, 2000). Maendeleo ya kidijiti yamebadilisha njia ya uwasilishaji wa nyimbo za Kiswahili za watoto kwa kiasi kikubwa. Hii ni kwa kuwa nyimbo nyingi za watoto zimewekwa na zinatumika kwenye vifaa vingine vingi vya kidijiti. Mara nyingi uwasilishwaji wake hautegemei kuwepo kwa hadhira, hali ambayo huwatenganisha fanani na hadhira yake. Na zile zilizo vitabuni nazo yampasa mtu ajue kusoma noti ili aweze kuimba akiwa akizisoma, ambapo nazo huwatenga hadhira kati ya wanaojua kusoma noti na wale wasiojua kuzisoma.

## 4.5 Huathiri Muktadha wa Utendaji wake

Nyimbo za watoto za Kiswahili za mwanzo zilikuwa zikiimbwa sambamba na wakati, majira pamoja na mazingira ya tukio. Kwa mfano, katika mazingira ya wakulima, wafugaji, wavuvi na kadhalika, nyimbo za watoto ziliimbwa zikiwa zimeelekezwa maudhui yake yaliyosawiri mazingira na wakati wa shughuli hizo. Mfano ni wimbo wa *Mama Huyo*:

8. Mama huyo
Katoka shambani
Na mkungu wa ndizi

Wimbo huu ulikuwa ukiimbwa na watoto wakati wa jioni wakimlaki mama yao akiwa anatoka katika shughuli za siku nzima za kilimo. Aidha, watoto walikuwa wakifurahia chakula alichorejea nacho mama akitokea shambani. Mfano mwingine ni wimbo wa *Sare Sare Maua*:

9. Sare sare maua,
Asiyejua kuchagua
Kabila lake Mzigua

Wimbo huu ulikuwa ukiimbwa wakati wa sherehe. Ulitumika kumkatisha tamaa mtu hasiyejua kuchagua vazi zuri la kuvaa kwenye sherehe fulani. Hivyo, nyimbo kama hizi na nyingine nyingi ziliimbwa na watoto kwa nyakati maalumu katika maisha yao. Nyimbo za watoto za Kiswahili katika kipindi hiki cha maendeleo ya teknolojia ya kidijiti huimbwa, hutazamwa, husomwa na kusikilizwa wakati wowote kulingana na matakwa ya fanani. Mara nyingi huwa tunazisikiliza nyimbo za Banza Stone (Ramadhani Masanja), *Yai Bovu* (data namba 3) na *Ukuti Ukuti* (data namba7), za Lukas Mkenda (Mr. Nice ) *Mama, Ana Do* na *Kidali Po* zikiimbwa, iwe nyakati za

jioni, mchana, msibani, harusini au sehemu nyingine. Hii inatuonesha kuwa nyimbo za watoto sasa zimeathiriwa na maendeleo teknolojia ya kidijiti.

**4.6 Hufifisha Utamaduni**

Kila jamii huwa na nyimbo za watoto, zenye kuangazia jadi na kaida za jamii husika. Jamii za wafugaji zilikuwa zikiimba nyimbo za jamii hiyo, watu wa pwani waliimba nyimbo zinazohusu mambo ya pwani na kadhalika. Kutokana na maendeleo ya teknolojia na kidijiti (na mwingiliano wa utamaduni) kumesambaa kaida, tabia na mienendo kadha wa kadha katika jamii zote ulimwenguni. Hivyo, maendeleo ya teknolojia ya kidijiti ulimwenguni, Tanzania ikiwemo, yameleta athari kubwa kiutamaduni, fasihi ikwemo ndani yake. Mathalan, kwa sasa watoto wengi wanaangalia televisheni na kutekwa na tamaduni za nje wanazojifunza humo. Hii huwafanya kujifunza mambo ya Kimagharibi na kusahau ya Kitanzania, ikiwemo fasihi simulizi (nyimbo zao).

**4.7 Hufanya Nyimbo za Watoto Kutobadilika kwa Wakati**

Maendeleo ya mfumo wa teknolojia ya kidijiti yanafanya kutokubadilika kwa fasihi ya watoto kulingana na mabadiliko yaliyopo katika jamii. Pamoja na umuhimu mkubwa wa vyombo hivi katika kuhifadhi nyimbo za watoto za Kiswahili, teknolojia hii imesababisha baadhi ya nyimbo za watoto kutobadilika kama ilivyo katika jamii za jadi. Kwa mfano wimbo *Maua Mazuri*:

10. Maua mazuri yapendeza x2
Ukiyatazama, yanameremeta
Hakuna limoja lisilopendeza x2

Wimbo huu tangu ulivyowekwa kwenye *You Tube* miaka kadhaa iliyopita, maua hayo yatasikika yakipendeza kuanzia Januari hadi Disemba, iwe kipindi cha mvua, jua, baridi, kiangazi na kadhalika, yenyewe yanapendeza tu. Uhalisia hapa haupo bali kukariri tu.

**4.8 Kudharauliwa kwa Ughanaji Asilia wa Nyimbo za Watoto**

Baada ya mabadiliko ya teknolojia ya kidijiti, watoto wamezama katika uimbaji wa kukariri maneno na midundo iliyorekodiwa na kutumika kwenye vifaa vingine vingi vya kidijiti, na wakadharau utambaji wa nyimbo zao walizokuwa wakizipenda na ambazo walikuwa wakiziimba na kuzighana moja kwa moja. Hili limesababisha kushuka kwa kiwango cha asili cha uchezaji wa nyimbo hizi. Kwa mfano, wimbo *Ukutu Ukuti* ulivyokuwa ukiimbwa na watoto katika michezo yao ulikuwa ukichezwa kama ilivyotakiwa. Baada ya kuingizwa katika nyimbo (muziki) za bongo fleva umebadilika kimahadhi na kuchukua mapigo ya ki-bongo fleva. Kwa kuwa nyimbo hizi zina umaarufu na kupendwa na wengi watoto kuziangalia nyimbo zao hizo pendwa katika televisheni, kompyuta na vifaa vingine vingi vya kidijiti zikichezwa kwa mitindo ya kibongo fleva, na wao huiga hivyo.

**4.9 Huunganisha Vizazi mbalimbali katika Jamii**
Maendeleo ya teknolojia ya kidijiti yamechangia kwa kiasi kikubwa nyimbo na michezo ya watoto kutumika na kutumiwa na wasanii mbalimbali katika tungo zao. Kama tulivyosema hapo awali baadhi ya wasanii wa muziki wa kizazi kipya (bongo fleva) hutumia nyimbo za watoto kama malighafi ya kuzalisha nyimbo/mashairi yao. Kwa kufanya hivyo huwasukuma wapenzi wa nyimbo hizo kukumbukia enzi ya utoto/ujana wao (taz. Omari, 2008). Aidha, nyimbo hizo huwavutia watoto katika kuzisikiliza na kuziimba.

**4.10 Huibua Vipaji na Kukuza Ubunifu wa Watoto**
Nyimbo hizo za watoto za Kiswahili tunazoziona zinarushwa katika vyombo vya kidijiti zimesaidia kwa kiasi fulani kukuza vipaji mbalimbali vya watoto ndani na nje ya jamii zetu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba watoto wetu wameweza kuona, kuiga na kutenda mambo mengine mengi yanayofanywa na watoto wengine duniani. Aidha, ni kwa kupitia teknolojiai hii, watoto wetu wameweza kuonesha vipaji vyao vizuri vya kiutendaji walivyokuwa navyo na kuweza kusaidiwa na jamii husika. Ndulute (1977) na Omari (2008) wanatudhihirishia kwamba watoto wanakuwa wabunifu wanapokuwa katika michezo yao, na hivyo kuweza kujulikana kwa watu wengine hata wanapokuwa watu wazima. Ingawa kwa upande mwingine, kuwepo kwa vifaa vya kidijiti kumesababisha kupoteza vipaji vya ubunifu vya watoto kwani kila kitu kimekwisharahisishwa kwao na teknolojia hii.

**4.10 Hueneza Kiswahili Ulimwenguni**
Maendeleo ya teknolojia ya kidijiti yamefanya kwa kiasi kikubwa nyimbo za watoto kutumika katika mitandao mbalimbali ya kijamii kama vile *You Tube*, *Facebook*, na *Twitter*. Kwa kufanya hivi si tu huzisambaza tamaduni mbalimbali zilizomo ndani yake bali pia hueneza lugha ya Kiswahili kwa watu wasioifahamu. Hii ni kutokana na nyimbo hizi kutumiwa pia na wasanii mbalimbali wa muziki wa kizazi kipya katika tungo zao. Wageni wanapoyasikia maneno ya nyimbo za watoto yaliyopangiliwa katika midundo muruwa ya kisasa, hufurahia kusikiliza bila wao wenyewe kujua kama wanajifunza lugha ya Kiswahili.

**4.11 Huchochea Ajira kwa Watoto**
Ajira za watoto limekuwa ni janga la kimataifa, hususani katika nchi zinazoendelea. Watoto wengi katika nchi hizi wamekuwa na kujiingiza au kuingizwa katika harakati za kutafuta fedha. Watoto wengi kwa kupitia vyombo vya habari, hususani wale wenye vipaji vizuri vya ubunifu walio na umri wa miaka 9 – 15 wameweza kupata ajira sehemu mbalimbali na kuacha masomo. Vilevile, baadhi ya watoto wameweza kupata ajira kwenye vituo vya televisheni na redio ili waweze kutumia vipaji vyao hivyo kutangaza vipindi mbalimbali. Wazazi, walimu na hata taifa wamesahau kwamba urithi mzuri unaomfaa mtoto ni elimu na sio kuhangaikia fedha ambayo sio msingi wa maendeleo.

## 5.0 Mustakabali wa Nyimbo za Watoto za Kiswahili katika Teknolojia ya Kidijiti

Baada ya kuangalia athari za maendeleo ya kidijiti katika nyimbo za watoto, hatuna budi kuangalia kwa kifupi mustakabali wa nyimbo hizo katika jamii. Tumeona mwingiliano wa kiutendaji katika tamaduni za Waswahili na zile za Kimagharibi. Kutokana na mwingiliano huo, tekinolojia ya kidijiti imekuwa ikisambaza na kueneza utumiaji wa zana mpya za kisasa, zilizorahisisha utungaji, uimbaji na utendaji wa fasihi ya watoto ya Kiswahili. Ni kwa kupitia teknolojia ya kudijitalisha nyimbo za watoto, uhalisia wa kiutendaji wa nyimbo hizo unaonekana kutetereka. Vilevile, ni kwa kupitia maendeleo ya kidijiti, utendaji wa nyimbo za watoto hadharani umeonekana kupoteza mwelekeo wake. Kwa upande wa usambazaji kumekuwa na usambazwaji mkubwa wa nyimbo nyingi za Kiswahili za watoto kupitia teknolojia ya kidijiti duniani. Nyimbo hizi zimekuwa zikisambazwa kuanzia kwenye ngazi ya kitaifa hadi ngazi ya kimataifa. Ni kwa kupitia ngazi za kitaifa na kimataifa ambapo wadau wa fasihi simulizi ya Kiswahili ya watoto wanapolishuhudia daraja jipya kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi ya watoto.

## 6.0 Hitimisho

Kwa kuhitimisha tunaweza kusema kuwa maendeleo ya teknolojia ya kidijiti yana athari kubwa katika maendeleo ya fasihi ya watoto. Athari hizo ni chanya na hasi. Tumeona kuwa maendeleo ya teknolojia ya kidijiti yameathiri pakubwa katika nyimbo za watoto kama vile utendaji, uhifadhi na umiliki. Aidha, makala haya yameonesha namna nyimbo za watoto zinavyotumika pia katika muziki/nyimbo nyingine kama vile za dansi na Bongo Fleva. Ieleweke kuwa ndani ya nyimbo hizi kuna ujumbe na matukio muhimu na hivyo nyimbo hizi ni utanzu muhimu wa fasihi simulizi kwa matumizi yetu ya sasa na ya baadaye.

## Marejeo


Balisidya, M. (1987), Tanzu za Fasihi Simulizi *Mulika No. 19*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research

King'ei, K. Na Kiovu, N.M. (2005), *Misingi ya Fasihi Simulizi,* Nairobi: Kenya Literature Bureau

Kiputiputi O. M (2011), *Kamusi Sanifu ya Kompyuta*. Dar es Salaam: TUKI

Machet, Sandra Olen and Thomas van der Walt (eds.) *Other World Other Lives: Children literature experiences vol. 1*. Pretoria: University of South Africa

Madeje, B.V. (1978), *Michezo ya Watoto Wadogo*. Tanzania Publishing House, Dar es Salaam

Matteru (1989), *Tanzu za Fasihi Similizi. Mulika* 19, Dar es Salaam: TUKI

Mbarouk, J.S. (1981), *Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Watoto.*Tasnifu M.A. Chuo Kikuu cha Zanzibar, (Haijachapishwa)

Mrikaria, S. E. (2007), 'Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya katika *Swahili Forum* 14: 197 – 206

Msokile, M. (1981), *Nafasi ya Nyimbo za Fasihi Simulizi katika Jamii Inayobadilika* katika *Semina ya Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Institute of Kiswahili Researh, Dar es Salaam

Mulokozi, M.M. (1975), "Ushairi wa Kiswahili na Ubantu hadi 1700: Maendeleo, Mabadiliko na Uhusiano na Ubantu na Mfumo wa Jamii: Unpublished paper, University of Dar es Salaam

______(1989), *Tanzu za Fasihi Simulizi*. A. M. Khamisi na J. S. Madumulla. *Mulika No. 21* uk. 1 - 24. Institute of Kiswahili Reseaıh, Dar es Salaam

______(1996), *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: OUT

Ndulute (1977), *The Place of Songs in Hehe Oral Literature*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (Haijachapishwa)

Ndumbaro, T.P (1981), *Jifunze kwa Nyimbo: Nyimbo za Shule ya Msingi*. Dar es Salaam: Longman Tanzania Limited

Ngara, E. (1990), *Ideology and Form in African Poetry*. London: James Currey

Ngure. A. (2003), *Fasihi Simulizi katika Shule za Sekondari*. Nairobi: Phonex Publishers Ltd

Omari, S. (2008), *Fasihi Simulizi na Jinsia: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto Tanzania*. Katika *Kiswahili Juz. 71*. Dar es Salaam: TUKI

Omari, S. (2009), 'Tanzanian Hip Hop Poetry As Popular Literature' Tasinifu Phd (Literature), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Samwel, M. (2012), Mabadiliko katika Majigambo: Uchunguzi wa Majigambo ya Jadi na ya Bongo Fleva, Tasnifu ya Uzamivu ( Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Senkoro, F.E.M.K (1996), *Viewing gender through Tanzania lullabies* in Myrna

Wamitila K. (2003), *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*, Nairobi: Focus Publication Ltd